JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA WA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A (GATCE) 2021

## URAIA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA WA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A (GATCE) 2021

# 612 URAIA

*Kimechapishwa na*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2021**

Haki zote zimehifadhiwa.

# YALIYOMO

DIBAJI ........ IV
1.0 UTANGULIZI ........ 1
2.0 TATHMINI YA KILA SWALI ........ 2
2.1 SEHEMU A: Maswali ya Majibu Mafupi (Taaluma na Utaalamu) ........ 2
2.1.1 Swali la 1: Dola ........ 2
2.1.2 Swali la 2: Dola ........ 4
2.1.3 Swali la 3: Utamaduni Wetu ........ 6
2.1.4 Swali la 4: Uchumi wa Tanzania ........ 9
2.1.5 Swali la 5: Dola ........ 12
2.1.6 Swali la 6: Uchambuzi wa Machapisho/Maandiko Muhimu ya Kufundishia na Kujifunzia Somo la Uraia ........ 15
2.1.7 Swali la 7: Zana za Kufundishia na Kujifunzia ........ 17
2.1.8 Swali la 8: Maandalizi ya Kufundisha Somo la Uraia ........ 19
2.1.9 Swali la 9: Utamaduni Wetu ........ 22
2.1.10 Swali la 10: Upimaji na Tathmini ........ 25
2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha (Taaluma) ........ 28
2.1.11 Swali la 11: Dola ........ 28
2.1.12 Swali la 12: Utamaduni Wetu ........ 34
2.1.13 Swali la 13: Uhusiano wa Kimataifa ........ 39
2.3 SEHEMU C: Maswali ya Insha (Utaalamu) ........ 44
2.1.14 Swali la 14: Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la Uraia ........ 44
2.1.15 Swali la 15: Uchambuzi wa Machapisho/Maandiko Muhimu ya Kufundishia na Kujifunzia Somo la Uraia ........ 48
2.1.16 Swali la 16: Zana za Kufundishia na Kujifunzia ........ 53
3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA ........ 57
4.0 HITIMISHO ........ 57
5.0 MAPENDEKEZO ........ 57
*KIAMBATISHO* ........ 59

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kutoa taarifa kuhusu ufaulu wa watahiniwa wa Mtihani wa Kuhitimu Ualimu Daraja la A kwa somo la Uraia. Taarifa hii imeandaliwa kutoa mrejesho wa ufaulu kwa wanachuo, wakufunzi, wakuu wa vyuo, wathibiti ubora, maafisa elimu, watunga sera na wadau wa elimu kwa ujumla.

Mtihani huu ni tathmini ya mwisho ambayo pamoja na mambo mengine, inaonesha mafanikio katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Uraia. Kimsingi majibu ya watahiniwa ni uthibitisho wa kipi mfumo wa elimu uliweza au ulishindwa kuwapa watahiniwa walipokuwa katika mafunzo ya Ualimu katika Daraja hili.

Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika somo hili ulikuwa mzuri. Ufaulu huu mzuri umechangiwa na watahiniwa kuwa na maarifa ya kutosha katika dhana mbalimbali zilizoulizwa, umahiri wa kutosha katika kuandika hoja zenye mtiririko mzuri kimantiki na umakini katika kusoma na kuelewa matakwa ya swali.

Uchambuzi uliyowasilishwa katika taarifa hii una lengo la kubainisha sababu zilizo wafanya watahiniwa kufanya vibaya au vizuri katika mtihani wao. Mrejesho huu utawawezesha viongozi wa elimu, wakuu wa vyuo, wakufunzi na wanachuo kuchukua hatua muafaka katika kuboresha ufaulu wa watahiniwa katika mitihani ijayo inayoandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

Mwisho, Baraza linapenda kuwashukuru maafisa mitihani na wadau wote waliohusika katika uchambuzi wa takwimu na kutayarisha taarifa hii.



Dkt. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

# 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa somo la Uraia uliandaliwa kwa kuzingatia muhtasari wa somo la Uraia wa mwaka 2009 na muundo wa mtihani wa mwaka 2017. Mtihani ulikuwa na maswali kumi na sita (16) na mtahiniwa alitakiwa kujibu jumla ya maswali kumi na nne (14) kutoka katika sehemu A, B na C. Sehemu A ilikuwa na maswali kumi (10) ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote na kila swali lilikuwa na alama nne (04). Sehemu B na C zilikuwa na maswali matatu (03) kila moja ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali mawili kutoka kila sehemu. Kila swali katika sehemu B na C lilikuwa na alama 15. Jumla ya alama kutoka katika sehemu A, B na C ilikuwa 100.

Ufaulu wa watahiniwa umegawanywa katika viwango vitatu ambavyo ni vizuri, wastani na hafifu. Ufaulu mzuri unaanzia alama 70 hadi 100, wastani alama 40 hadi 69 na hafifu alama 0 hadi 39. Aidha, chati za viwango vya ufaulu zimeambatishwa ili kufafanua ufaulu wa watahiniwa ambapo rangi ya kijani inawakilisha ufaulu mzuri, rangi ya njano ufaulu wa wastani na rangi nyekundu inawakilisha ufaulu hafifu.

Takwimu zinaonesha kuwa somo hili lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kuwa kati ya watahiniwa 4,332 waliofanya mtihani, watahiniwa 4,330 (99.95%) walifaulu kwa kupata wastani wa alama 40 na zaidi na watahiniwa 2 (0.05%) walifeli. Ufaulu huu umepungua kwa asilimia 0.03 ikilinganishwa na ufaulu wa mwaka 2020, ambapo asilimia 99.98 ya watahiniwa waliofanya mtihani walifaulu.

Taarifa hii inachambua maswali ya watahiniwa yaliyojibiwa vizuri, kwa wastani na hafifu ili kukuza kiwango cha ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Uraia. Sampuli za majibu zimeambatishwa ili kuonesha uwezo na udhaifu katika majibu ya watahiniwa. Vilevile, taarifa inaonesha sababu zilizofanya watahiniwa kupata alama za juu na wengine kupata alama hafifu kupitia majibu ya maswali kwa mada mbalimbali. Inatarajiwa kuwa uchambuzi huu utasaidia kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Uraia ili kuboresha zaidi ufaulu wa watahiniwa katika mitihani ijayo.


## 2.0 TATHMINI YA KILA SWALI

### 2.1 SEHEMU A: Maswali ya Majibu Mafupi (Taaluma na Utaalamu)

Katika sehemu hii ufaulu wa watahiniwa uligawanyika katika makundi matatu ambapo, mtahiniwa alikuwa na ufaulu hafifu endapo alipata kuanzia alama 0 hadi 1.5; ufaulu wa wastani endapo alipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na alikuwa na ufaulu mzuri endapo alipata kuanzia alama 3 hadi 4.

#### 2.1.1 Swali la 1: Dola

Swali lilimtaka mtahiniwa kuainisha majukumu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutumia hoja nne. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa asilimia 98.9 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na. 1.





**Chati Na. 1:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 1*

Chati Na. 1 inaonesha kuwa, asilimia 1.1 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata kuanzia alama 0 hadi 1; asilimia 3.5 walipata alama 2 na asilimia 95.4 walipata kuanzia alama 3 hadi 4.

Uchambuzi unaonesha kuwa, watahiniwa wengi (95.4%) waliopata kuanzia alama 3 hadi 4 walijibu swali hili kwa usahihi jambo linaloonesha kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Dola hususan kipengele cha Majukumu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na


walielewa matakwa ya swali. Mfano wa majibu sahihi yaliyoainishwa ni kama ifuatavyo; *kuratibu na kusimamia utendaji wa shughuli mbalimbali za kimaendeleo, kuandaa na kusimamia sera mbalimbali za maendeleo, kuboresha miundombinu, kusimamia amani na utulivu wa nchi, kudumisha ushirikiano na mataifa mengine* na *kulinda na kuheshimu haki za binadamu*. Kielelezo Na. 1.1 ni mfano wa jibu la mtahiniwa aliyepata alama za juu katika swali hili.


1. (i) Kusimamia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimaendeleo
(ii) Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao
(iii) Kuboresha huduma za jamii ikiwa ni pamoja na sekta ya elimu, sekta ya afya
(iv) Kutatua migogoro mbalimbali kati ya wananchi na taasisi mbali mfano taasisi ya fedha au machinika mbalimbali.

Kielelezo Na. 1.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 1

Takwimu zinaonesha kuwa asilimia 3.5 ya watahiniwa waliopata ufaulu wa wastani, hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana iliyoulizwa hivyo walitoa majibu pungufu ya matatu na wengine walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Mtahiniwa mmoja kwa mfano kwenye majibu yake alichanganya kazi za wakuu wa idara fulani au kazi za dawati la polisi au vitengo vya haki za binadamu kwa kuandika majibu kama; *kufuatilia uchapakazi wa kila mtumishi* na *kusimamia unyasanyaji wa kijinsia*, majibu ambayo ni dhaifu kuelezea majukumu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hivyo alipata alama 2.

Kwa upande mwengine, watahiniwa wachache (1.1%) waliopata ufaulu hafifu kati yao asilimia 0.6 walidhihirisha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana iliyoulizwa, hivyo walitoa jibu moja sahihi au kuandika majibu dhaifu mawili yaliyosababisha kupata alama 1. Asilimia 0.5 ya waliopata alama 0 baadhi yao walikosa maarifa kabisa kuhusu dhana iliyoulizwa na wengine walichanga maarifa kwa kuandika majibu yaliyo kinyume na matakwa ya swali kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 1.2.




| | |
|---|---|
| 1 | i) kutunga sheria |
| | ii) kuwasilisha bajeti. |
| | iii) kumchagua Spika wa bunge. |
| | iv) kumshauri raisi. |

Kielelezo Na. 1.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 1

Katika Kielelezo Na. 1.2 mtahiniwa aliainisha kazi za Bunge na kuchanganya na moja miongoni mwa majukumu ya Wizara bila maelezo yeyote badala ya kuainisha majukumu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hivyo alipata alama 0.

### 2.1.2 Swali la 2: Dola


Swali hili lilimtaka mtahiniwa kufikiria endapo amepangiwa kufundisha mada ndogo ya *Haki za Raia* kwa wanafunzi wa Darasa la Sita, kwa kutoa hoja nne abainishe mambo atakayosisitiza juu ya umuhimu wa kuzingatia haki za raia katika Dola. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa asilimia 70.2 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na. 2.




**Chati Na. 2:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 2*


Chati Na. 2 inaonesha kuwa, asilimia 29.8 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata kuanzia alama 0 hadi 1; asilimia 4.9 walipata alama 2 na asilimia 65.3 walipata kuanzia alama 3 hadi 4.

Watahiniwa waliopata kuanzia alama 3 hadi 4 walibainisha umuhimu wa kuzingatia haki za raia katika Dola, kwa kutoa majibu matatu hadi manne. Watahiniwa hao walielewa matakwa ya swali na walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana nzima ya Dola hususan kipengele cha Uraia na hivyo walitoa majibu sahihi kama*; hufanya raia kuwa huru kuishi na kuabudu, huwafanya raia kujiunga na vyama mbalimbali vya siasa, watu kupata fursa ya kushiriki kikamilifu katika mambo ya kijamii na kiuchumi hivyo kuiletea nchi maendeleo* na *raia kuwa huru kushiriki katika uchaguzi wa kupata viongozi mbalimbali.* Kielelezo Na. 2.1 ni moja ya mfano wa jibu la mtahiniwa aliyepata ufaulu mzuri katika swali hili.


2. (i) Husaidia kuishi kwa amani na usalama.
(ii) Husaidia kuleta maendeleo.
(iii) Husaidia kuongeza uwajibikaji wa raia pale anapofahamu haki zake.
(iv) Husaidia kudumisha umoja na mshikamano katika nchi kupitia haki za raia.

Kielelezo Na. 2.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 2

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, asilimia 29.8 ya watahiniwa walipata ufaulu hafifu ambapo asilimia 3.0 kati yao walipata alama 1 jambo linaloashiria walikuwa na maarifa hafifu kuhusu dhana iliyoulizwa. Asilimia 26.8 ya watahiniwa kwenye kundi hili walipata alama 0, jambo linaloonesha hawakuelewa matakwa ya swali, hivyo waliandika majibu kinyume na dhana iliyoulizwa. Mtahiniwa mmoja kwa mfano aliandika haki za raia katika jamii au Dola kwa kutoa majibu kama; *haki ya kupiga kura*, *haki ya kuishi*, *haki ya kusikilizwa* na *haki ya kuchagua Raisi*. Mtahiniwa mwingine kwenye kundi hili aliandika wajibu wa raia katika jamii au Dola kwa kutoa majibu kama; *kuwa mchapa* kazi, *kuwapenda watu wengine* na *kusalimia wakubwa*. Kielelezo Na. 2.2 ni mfano wa jibu la mtahiniwa aliyeshindwa swali hili.



02. i) Mtoto kupewa huru wakuchagua chama chochote anachokitaka yeye kwa maamuzi yake mwenyewe.

ii) Mtoto kupewa haki ya kusoma na kuanzishwa shule pale tu anapofikisha miaka yakuanza awali.

iii) Mtoto kupewa mahitaji yake ya msingi kama chakula mavazi na maradhi pale anapokuwa na uhitaji wa vitu hivyo.

iv) Mtoto kuwa na uwezo wakuchangia pale panapokuwa na shida yoyote.


Kielelezo Na. 2.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 2

Katika Kielelezo Na. 2.2 mtahiniwa aliandika haki za mtoto katika familia na jamii badala ya kubainisha umuhimu wa kuzingatia haki za raia katika Dola, hivyo alipata alama 0.

Aidha, asilimia 4.9 ya watahiniwa walikuwa na ufaulu wa wastani. Ufaulu huo ni matokeo ya watahiniwa kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana iliyoulizwa hivyo kuandika majibu pungufu na wengine kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Mtahiniwa mmoja kwa mfano alichanganya majibu ambayo si sahihi kama ifuatavyo; *kujua jinsi haki za binadamu zinavyolindwa na Dola* na *kulinda na kutetea nchi*; hivyo alipata alama za wastani.

### 2.1.3 Swali la 3: Utamaduni Wetu


Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha mila zinazo changia kuenea kwa maambukizi ya UKIMWI kwa kutumia hoja nne. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa asilimia 81.4 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na. 3




**Chati Na. 3:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 3*

Chati Na. 3 inaonesha kuwa, asilimia 18.6 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata kuanzia alama 0 hadi 1; asilimia 37 walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na asilimia 44.4 walipata kuanzia alama 3 hadi 4.

Asilimia 44.4 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 3 hadi 4 katika swali hili kwa kuwa walielewa matakwa ya swali na walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya Mila na Desturi Zinazochangia Ueneaji wa UKIMWI. Watahiniwa wengi katika kundi hili walibainisha mila tatu hadi nne zinazochangia kuenea kwa maambukizi ya UKIMWI. Baadhi ya majibu sahihi yalikuwa: *kurithi wajane, ukeketaji wa wanawake au wasichana na tohara ya wanaume yenye kutumia kifaa kimoja, utakaso wajane, ndoa za utotoni, ndoa za wake wengi na ndoa za lazima.* Kielelezo Na. 3.1 ni mfano wa jibu la mtahiniwa aliyebainisha mila zinazochangia kuenea kwa maambukizi ya UKIMWI kwa usahihi.


3 i) Ukeketaji. mfano utumiaji wa vifaa vya kukeketea
kwa kuchangia mtu zaidi ya mmoja.

ii) Kurithi wajane. Inapelekea maambukizi ya UKIMWI
endapo mrithi au mrithiwa ana maambukizi.


iii) Ndoa za mitala. Mfano mtu kuwa na mke zaidi
ya mmoja endapo kati ya hao wana
wake au mume ana maambukizi atasababisha
wengine wote kupata maambukizi ya UKIMWI.

iv) Kutakasa wajane. Endapo mjane akawa na
maambukizi atasababisha mtakasaji kupata ma
mbukizi hayo. hivyo basi mwanaume aliye
mtakasa akiwa na wanawake wengine maa
mbukizi yataendelea kusambaa.

Kielelezo Na. 3.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 3

Asilimia 37 ya watahiniwa waliopata alama za wastani katika swali hili walikuwa na mapungufu mbalimbali katika majibu yao kama: kuandika majibu pungufu kinyume na matakwa ya swali, kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi na kurudia jibu, mtahiniwa mmoja kwa mfano aliandika; *kuwa na wake wengi* na kisha kurudia *mitala*. Mtahiniwa mwingine aliandika; *ukeketaji* na *tohara*, kama majibu tofauti bila kuainisha ni zenye kutumia kifaa kimoja, hivyo kukosa alama.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliopata kuanzia alama 0 hadi 1.5, baadhi yao (16.2%) walishindwa kukidhi matakwa ya swali kwa kutoa majibu pungufu na yenye udhaifu hivyo kupata alama 0.5 hadi 1.5. Wengine (2.4%) waliopata alama 0, kati yao wapo walioacha nafasi wazi baada ya kuandika namba ya swali na wengine waliandika majibu kinyume na matakwa ya swali. Mtahiniwa mmoja kwa mfano aliandika majibu yasiyo sahihi kama; *wahehe, warangi, wachaga* na *wasukuma*. Mtahiniwa mwingine katika kundi hili aliandika; *kimasai*, *kisukuma*, *nyaturu* na *wakurya*. Kwa ujumla, watahiniwa wengi waliopata ufaulu hafifu katika swali hili walichanganya mila zinazochangia kuenea kwa maambukizi ya UKIMWI na makabila yanayojihusisha na mila zinazochangia maambukizi ya UKIMWI kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 3.2.



3. (i) Mila za wamasai
(ii) Mila za wakurya
(iii) Mila za wazanaki
(iv) Mila za watanga

Kielelezo Na. 3.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 3

Katika Kielelezo Na. 3.2 mtahiniwa aliandika makabila aliyodhani yanajihusisha na mila zinazochangia kuenea kwa maambukizi ya UKIMWI katika jamii ya Kitanzania badala ya kubainisha mila zinazochangia kuenea kwa maambukizi ya UKIMWI.

### 2.1.4 Swali la 4: Uchumi wa Tanzania


Swali lilimtaka mtahiniwa aeleze kwa kifupi umuhimu wa utaalamu katika ukuaji wa uchumi nchini Tanzania kwa kutoa hoja nne. Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa asilimia 95.9 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na.4.




**Chati Na. 4:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 4*

Chati Na. 4 inaonesha kuwa, asilimia 4.1 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5; asilimia 9.2 walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na asilimia 86.7 walipata kuanzia alama 3 hadi 4.

Watahiniwa wengi (86.7%) waliopata kuanzia alama 3 hadi 4 walieleza kwa kifupi hoja tatu hadi nne za umuhimu wa utaalamu katika ukuaji wa uchumi nchini Tanzania. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ndogo ya Mambo Yanayochangia Kukua au Kuporomoka kwa Uchumi na walielewa matakwa ya swali. Baadhi ya majibu sahihi katika swali hili yalikuwa; *utungaji wa sera mbalimbali, uwekaji wa mipango katika uchumi, utendaji wenye ujuzi katika miradi au biashara ambao hukuza uchumi katika nchi, matumizi sahihi ya fursa, utafutaji wenye tija wa masoko kwa bidhaa mbalimbali zinazozalishwa ndani ya nchi hata nje ya nchi, utungaji wa sheria zitakazolinda mazingira na rasilimali* na *kufanya tafiti mbalimbali za kimaendeleo*. Kielelezo Na. 4.1 ni mfano wa jibu sahihi katika swali hili.


4. (i) Husaidia katika kupanga bajeti mbalimbali za miradi ya kimaendeleo hasa katika sekta ya uchumi.

(ii) Husaidia katika kutunga sera za uchumi ambazo huchochea maendeleo ya kiuchumi

(iii) Husaidia katika kutoa ushauri kwa serikali juu ya maendeleo ya kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuishauri serikali namna ya kutatua changamoto zinazoikumba sekta ya uchumi nchini


(iv) Husaidia kutoa elimu kwa wananchi juu ya kuboresha sekta mbalimbali hasa zinazohusika na ukuaji wa viwanda mfano. Kilimo, uvuvi, ufugaji viwanda. Uchimbaji madini.

Kielelezo Na. 4.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 4

Asilimia 9.2 ya watahiniwa waliopata alama za wastani walielewa matakwa ya swali isipokuwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu umuhimu wa utaalamu katika ukuaji wa uchumi nchini Tanzania, hivyo walishindwa kutoa majibu yote manne kwa usahihi. Baadhi kati yao walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Mtahiniwa mmoja kwa mfano pamoja na

kuandika majibu sahihi alichanganya na majibu yasiyo sahihi kama; *kuboresha uvumbuzi* na *kuboresha mawasiliano*.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache (4.1%) waliopata kuanzia alama 0 hadi 1.5, baadhi yao (2.1%) walikuwa na maarifa hafifu kuhusu dhana husika na hivyo kutoa majibu dhaifu yalisababisha kupata alama 0.5 hadi 1.5. Wengine (2.0%) waliopata alama 0, wengi walidhihirisha kutokuwa na maarifa kuhusu dhana ya Utaalamu katika ukuaji wa uchumi nchini Tanzania na wengine hawakuelewa matakwa ya swali. Mtahiniwa mmoja kwa mfano aliandika majibu yasiyo sahihi kama; *kurahisisha kupata ajira*, *husaidia katika matumizi ya teknolojia* na *husaidia kuzalisha malighafi*. Mtahiniwa mwingine katika kundi hili aliandika majibu yasiyo sahihi kama; *kuenea kwa wataalamu*, *kuenea kwa teknolojia* na *kudumisha umoja na mshikamano*. Kielelezo Na. 4.2 ni mfano wa jibu la mtahiniwa aliyepata alama 0.



4. Utaalamu, ni ile hali ya mtu kutoa ujuzi jau ya ja mbo flani
Zifuatazo ni umuhimu wa utaalam katika ukuaji wa uchumi nchini
husaidia kujua Idadi ya watu, ukiwa unajua sera ya nchi ni rahisi sana ku jua Idadi
husaidia kujua migogoro katika nchi katika nchi ya Tanzania unatakiwa ujue migogoro ya aina mbalimbali
inasaidia kujua mbinu mbalimbali, mtu akikiwa na mbinu yeyote inahisi kukosa umuhimu kama huo
husaidia kujua sera ya nchi, unatakiwa ukitaka kujua sera ya nchi unataki uje sera ya nchi na kuweza kuitumia
Hitimisho, zifuatazo ndio zo umuhimu wa kufundisha na kujifunza somo la uraia.

Kielelezo Na. 4.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 4

Katika Kielelezo Na. 4.2 mtahiniwa alieleza umuhimu wa kuwa mtaalamu katika mambo mbalimbali ya nchi badala ya kueleza kwa ufupi umuhimu wa utaalamu katika ukuaji wa uchumi nchini Tanzania. Vilevile mtahiniwa alidhihirisha kutokuwa na maarifa kuhusu aina ya maswali kwa kuandika utangulizi na hitimisho kwenye swali la majibu mafupi.

### 2.1.5 Swali la 5: Dola

Swali lilimtaka mtahiniwa akiwa kama mwalimu mahiri wa somo la Uraia, kuelezea kwa kifupi mambo manne ya kuzingatia katika kuhusisha Katiba ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania na mada inayofundishwa. Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu kwa kuwa ni asilimia 5.4 pekee ya watahiniwa ndiyo walipata kuanzia alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na.5.





**Chati Na. 5:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 5*

Chati Na. 5 inaonesha kuwa, asilimia 94.6 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5; asilimia 2.3 walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na asilimia 3.1 walipata kuanzia alama 3 hadi 4.


Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa wengi (94.6%) walishindwa swali hili. Baadhi yao (4.6%) waliandika hoja sahihi moja au waliandika hoja dhaifu mbili na hivyo kupata alama za chini. Wengine (90%) walipata alama 0 kwa kuwa hawakuelewa matakwa ya swali au hawakuwa na maarifa

kuhusu dhana iliyoulizwa. Mtahiniwa mmoja kwa mfano aliandika majibu ambayo si sahihi kama; *kutambua lengo*, *kutambua aina za katiba* na *kutambua matumizi ya katiba*. Kielelezo Na. 5.1 ni mfano wa jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kueleza kwa usahihi mambo manne ya kuzingatia katika kuhusisha Katiba ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania na mada inayofundishwa.


5. Mambo yakuzingatia katika kuhusisha katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mada inayofundishwa.
i) katiba womwayo ndiyo katiba iliyopo
ii) katiba Hutungwa
iii) Husimamiwa
iv) katiba hufatwa na kutekelezwa.

Kielelezo Na. 5.1: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 5


Katika Kielelezo Na. 5.1 mtahiniwa aliainisha sifa za Katiba badala ya kueleza mambo ya kuzingatia katika kuhusisha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mada inayofundishwa. Kielelezo Na. 5.2 ni mfano mwingine wa jibu la mtahiniwa aliyeshindwa swali hili.


5 Mambo ya kuzingatia katika kuhusianisha — Katiba ya Jamhuri ya muungano wa Tanzania — na mada inayofundishwa.
(i) uchaguzi huru na wa haki
(ii) uwepo wa vyama vingi
(iii) utawala wa kisheria
(iv) uhuru wa kiuchumi na uwajibikaji.

Kielelezo Na. 5.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 5

Katika Kielelezo Na. 5.2 mtahiniwa aliandika misingi ya kidemokrasia badala ya kueleza mambo ya kuzingatia katika kuhusisha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mada inayofundishwa, hivyo alipata alama 0.

Kwa upande mwingine, asilimia 3.1 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 3 hadi 4 kwa kuwa walieleza kwa kifupi mambo matatu hadi manne ya kuzingatia katika kuhusisha Katiba ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania na mada inayofundishwa kwa kuandika majibu kama yafuatayo: *kuandaa nakala za kutosha za vipengele vya katiba unavyotakiwa kufundisha kwa kuhusisha na mada unayofundisha, kupitia kwa makini vipengele vya katiba, kuandaa kazi za darasani* na *kuwa karibu na wanafunzi wako wakati wa majadiliano*. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya Misingi ya Ufundishaji wa somo la Uraia na walielewa matakwa ya swali. Kielelezo Na. 5.3 ni mfano wa jibu la mtahiniwa aliyepata ufaulu mzuri katika swali hili.



5. (i) Ili kuhusisha ni lazima kutafuta matini ya kutosha ili kulinganisha na mada za uraia.
(ii) Kupitia vipengele vilivyopo kwenye katiba kwa kulinganisha na mada kwa makini.
(iii) Kuwaeleza wanafunzi kutafuta katiba na kulinganisha na mada hizo.
(iv) Kuwa karibu na wanafunzi wakati wanapojadili kuhusiana na mada kwa kulinganisha na katiba ili kama wakikosea katika kulinganisha mwalimu awaelekeze.

Kielelezo Na. 5.3: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 5

Watahiniwa wachache (2.5%) waliokuwa na ufaulu wa wastani walikuwa na mapungufu mbalimbali katika majibu yao kama; kuchaganya majibu sahihi na yasiyo sahihi au kutoa majibu pungufu ya matatu na hivyo walipata alama za wastani. Mtahiniwa mmoja kwa mfano alichanganya hoja zisizo sahihi kwenye majibu yake kwa kuandika; *kuangalia kama kuna dhana tata katika mada* na *kutafuta maarifa ya awali ya wanafunzi*.

### 2.1.6 Swali la 6: Uchambuzi wa Machapisho/Maandiko Muhimu ya Kufundishia na Kujifunzia Somo la Uraia

Swali lilimtaka mtahiniwa kutoa hoja nne, kuelezea umuhimu wa muhtsari wa somo la Uraia kwa mwalimu tarajali anayejiandaa na mafunzo kwa vitendo. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa asilimia 98.3 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na. 6.





**Chati Na. 6:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 6*

Chati Na. 6 inaonesha kuwa, asilimia 1.7 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5; asilimia 2.5 walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na asilimia 95.8 walipata kuanzia alama 3 hadi 4.

Watahiniwa wengi (95.8%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4 kwa sababu walikidhi matakwa ya swali kwa kuelezea hoja tatu hadi nne kuhusu umuhimu wa muhtsari wa somo la Uraia kwa mwalimu tarajali anayejiandaa na mafunzo kwa vitendo. Sababu nyingine ya ufaulu ni kuwa dhana ya muhtasari hufundishwa pia katika masomo mengine wanayosoma ya ufundishaji, hivyo watahiniwa wengi walihawilisha maarifa. Baadhi ya majibu sahihi yaliyotolewa na wanafunzi hao ni; *humsaidia kuandaa azimio la kazi, humsaidia kuchagua mbinu/njia za kufundishia kulingana na mazingira ya shule, humwezesha kufahamu malengo na ujuzi anaotarajiwa kuwajengea wanafunzi, humwezesha kupata picha ya mada atakazofundisha*


na *humwezesha kuandaa zana za kufundishia*. Kielelezo Na. 6.1 ni mfano wa jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri kwa kuelezea umuhimu wa muhtsari wa somo la Uraia kwa mwalimu tarajali anayejiandaa na mafunzo kwa vitendo kwa hoja nne.


6. (i) Humsaidia mwalimu kuandaa azimio la kazi.
(ii) Humsaidia mwalimu kufundisha katika mpangilio (mtiririko maalumu).
(iii) Humsaidia mwalimu katika suala zima la uandaaji wa zana.
(iv) Humrahisishia mwalimu katika uandaaji wa vipindi na idadi ya mada atakazofundisha

Kielelezo Na. 6.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 6

Aidha, asilimia 2.5 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 kwa sababu waliandika majibu pungufu ya matatu au walirudia jibu na wengine walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Mtahiniwa mmoja kwa mfano alichanganya majibu yasiyo sahihi kama ifuatavyo; *humsaidia mwalimu kupata shughuli ndogo* na *humsaidia mwalimu kuingia darasani*; hoja ambazo ni dhaifu katika kuelezea umuhimu wa muhtasari kwa mwalimu.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa waliopata kuanzia alama 0 hadi 1.5, baadhi yao (0.7%) walikuwa na maarifa hafifu kuhusu dhana nzima ya Muhtasari wa somo la Uraia hivyo kuorodhesha jibu moja au mawili yenye dosari zilizosababisha kupata alama 1 au 1.5. Watahiniwa wengine (1%) waliopata alama 0 hawakuelewa matakwa ya swali, hivyo kutoa majibu yasiyo sahihi. Mtahiniwa mmoja kwa mfano aliandika majibu yasiyo sahihi kama; *humsaidia mwalimu kujibu maswali atakayoulizwa na watoto, humsaidia mwalimu kusahihisha kazi za watoto* na *humsaidia mwalimu kupata kazi*. Aidha, watahiniwa wengine kwenye kundi hili waliandika namba na kuacha nafasi wazi. Kielelezo Na. 6.2 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyepata ufaulu hafifu katika swali hili.




| | |
|---|---|
| 6 | i) Kutambua haki za binadamu |
| | ii) Kutambua wajibu wa kila raia |
| | iii) Kutambua Serikali ya Tanzania |
| | |

Kielelezo Na. 6.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali 6

Katika Kielelezo Na. 6.2 mtahiniwa alieleza umuhimu wa somo la Uraia badala ya umuhimu wa Muhtasari wa somo la Uraia kwa mwalimu tarajali anayejiandaa na mafunzo kwa vitendo na hivyo alipata alama 0.

### 2.1.7 Swali la 7: Zana za Kufundishia na Kujifunzia


Swali lilimtaka mtahiniwa kutoa hoja nne kuonesha kwa kifupi mbinu atakazozitumia katika kupata zana za kufundishia na kujifunzia endapo atapangiwa kufundisha somo la Uraia katika shule ya Msingi baada ya kuhitimu mafunzo yake ya Ualimu. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa asilimia 92 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na. 7.




**Chati Na. 7:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 7*

Chati Na. 7 inaonesha kuwa, asilimia 8 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata kuanzia alama 0 hadi 1; asilimia 8 walipata alama 2 na asilimia 84 walipata kuanzia alama 3 hadi 4.

Ufaulu mzuri katika swali hili ulisababishwa na asilimia 84 ya watahiniwa kupata kuanzia alama 3 hadi 4. Watahiniwa hao walikidhi matakwa ya swali kwa kutaja mbinu tatu hadi nne zinazotumika kupata zana za kufundishia na kujifunzia kwa kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya Zana za Kufundishia na Kujifunzia. Baadhi ya majibu sahihi yaliyotolewa na watahiniwa hao ni; *kununua, kutengeneza, kuazima, kufaragua, kukodi kutoka kwenye taasisi mbalimbali* na *kutumia mazingira.* Kielelezo Na. 7.1 ni mfano wa jibu sahihi la mtahiniwa katika swali hili.



7 (a) kutengeneza zana; Nitatumia makun zi yaliyopo katika mazingira ili Kutengeneza zana mbalimbali.

(b) Kuazima zana; nitaweza kuazima katika Shule jirani ili kuweza kufanikisha ufundishaji. au kuazima kwa walimu wengine.

(c) Kununua zana; Nitaweza kununua zana mbalimbali katika sehemu wanazouza.


(d) kufaragua zana; ninaweza kufaragua vitu mbalimbali kutokana na mazingira ya ufundishaji.

Kielelezo Na. 7.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 7

Asilimia 8 ya watahiniwa waliopata kuanzia alama 2 hadi 2.5 walionesha mapungufu mbalimbali katika majibu yao. Mapungufu hayo yalikuwa ni; kuandika majibu pungufu, kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi na kurudia majibu. Mtahiniwa mmoja kwa mfano aliandika hoja ya *kuchonga na kutengeneza* bila ya kujua kuwa majibu haya mawili yanaingia kwenye kundi la *kutengeneza*.

Kwa upande mwingine, asilimia 8 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 0 hadi 1 ambapo baadhi yao (7.3%) walitaja mbinu zisizozidi mbili na wengine walirudia hoja katika majibu yao, hivyo walipata alama 1.

Mtahiniwa mmoja kwa mfano aliandika; *kufinyanga*, *kutengeneza*, *kusuka* na *kufuma*; bila kujua hoja hizi zote zinaingia kwenye kundi la kutengeneza. Wengine (0.7%) waliopata alama 0 walishindwa kutaja mbinu sahihi hata moja. Watahiniwa hao hawakuelewa matakwa ya swali na hivyo waliandika majibu tofauti na kilichoulizwa. Mtahiniwa mmoja kwa mfano alitaja mbinu za kutunza zana kwa kutoa majibu kama; *kupaka rangi*, *kuweka kwenye fremu* na *kuhifadhi juu*. Kielelezo Na. 7.2 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kueleza kwa usahihi mbinu zinazoweza kutumika katika kupata zana za kufundishia na kujifunzia.



7. i/. mbinu ya mrchezo
ii/. mbinu ya nyimbo
iii/. mbinu ya maigizo
iiii/. mbinu ya hadithi

Kielelezo Na. 7.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 7

Katika Kielelezo Na. 7.2 mtahiniwa alitaja mbinu za kufundishia zinazotumika katika madarasa ya Elimu ya Awali kama; *mbinu ya nyimbo,* na *mbinu ya hadithi* badala ya mbinu za kupata zana za kufundishia na kujifunzia somo la Uraia kama; *kutengeneza*, *kufaragua* na *kuazima*.

### 2.1.8 Swali la 8: Maandalizi ya Kufundisha Somo la Uraia

Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa kutoa mifano dhana ya vitendo vya ufundishaji na vitendo vya ujifunzaji kama zinavyotumika katika azimio la kazi la somo la Uraia. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa asilimia 94.8 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na. 8.




**Chati Na. 8:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 8*


Chati Na. 8 inaonesha kuwa, asilimia 5.2 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata kuanzia alama 0 hadi 1; asilimia 4.8 walipata alama 2 na asilimia 90 walipata kuanzia alama 3 hadi 4.

Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa wengi (90%) walipata ufaulu mzuri kwa sababu walieleza kwa mifano dhana ya vitendo vya ufundishaji na ujifunzaji hivyo walipata alama 3 hadi 4 kutokana na usahihi wa maelezo ya kila mmoja. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu azimio la kazi na muundo wake na walielewa matakwa ya swali. Majibu sahihi katika swali hili yalikuwa kama ifuatavyo:

(a) *Vitendo vya ufundishaji ni kipengele kinachoonesha shughuli za mwalimu kama mwezeshaji wa mwanafunzi ili aweze kujijengea uwezo wa kujitegemea na kufikiri. Kwa mfano kugawa kazi kwenye makundi ili wanafunzi wajadiliane darasani*; na

(b) *Vitendo vya ujifunzaji ni sehemu ambayo mwanafunzi ndiye mtendaji mkuu. Vitendo vya ujifunzaji ndio vitendo muhimu vinavyosaidia kukuza ujuzi. Kwa mfano, wanafunzi kushiriki katika majadiliano kwenye vikundi vyao vya kazi na kisha kuwasilisha darasani*.

Kielelezo Na. 8.1 ni mfano wa jibu sahihi la mtahiniwa ambaye alieleza kwa kutoa mifano dhana ya vitendo vya ufundishaji na ujifunzaji.



08. (a) Vitendo vya ufundishaji
- Ni shughuli mbalimbali ambazo mwalimu huziandaa ili kuwawezesha wanafunzi wakati wa ufundishaji. Mfano mwalimu kuwawezesha wanafunzi kuimba wimbo wa Taifa.

(b) Vitendo vya ujifunzaji.
- Ni shughuli anazotegemea mwalimu kuziona kwa wanafunzi wake wakizitenda au kuzifanya wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la uraia. Mfano. Wanafunzi kuimba wimbo wa Taifa.

Kielelezo Na. 8.1 Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 8

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa ufaulu wa wastani katika swali hili ulisababishwa na asilimia 4.8 ya watahiniwa kushindwa kutoa mifano katika maelezo yao au kutoa maelezo ya upande mmoja na hivyo kupata alama 2. Mtahiniwa mmoja kwa mfano alikosa upande mmoja wa swali kwa kuwa aliandika; *vitendo vya kufundishia ni kitendo ambacho mwanafunzi anatakiwa kuwa amekifahamu*, bila kutoa mfano wowote, hivyo alipata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, asilimia 5.2 ya watahiniwa waliopata ufaulu hafifu, baadhi yao (1.4%) walikuwa na maarifa hafifu kuhusu dhana iliyoulizwa hivyo kutoa majibu dhaifu yaliyosababisha kupata alama 1. Asilimia 3.8 ya waliobakia walipata alama 0. Baadhi yao walishindwa kuelewa matakwa ya swali na hivyo kutoa majibu kinyume na matakwa ya dhana iliyoulizwa na wengine hawakuwa na maarifa kuhusu dhana husika. Mtahiniwa mmoja kwa mfano aliandika majibu ambayo si sahihi kama; Vitendo vya ufundishaji *ni pale watoto kadhaa wakiwa wameelewa somo kwa kiasi fulani* na Vitendo vya ujifunzaji *ni pale mwalimu anapotumia mbinu kufundisha*. Aidha, baadhi ya watahiniwa hao walichanganya majukumu ya mwalimu na mwanafunzi katika vitendo hivyo. Kielelezo Na. 8.2 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kuelezea kwa kutoa mifano dhana ya vitendo vya ufundishaji na ujifunzaji kama zinavyotumika katika azimio la kazi la somo la Uraia.



8. a/ Vitendo vya Ufundishaji.
[illegible] ya kipindi cha [illegible] 40 [illegible]
wanafunzi wote wajue maana ya Uraia na umu
himu wa uraia.
b/ Vitendo vya ujifunzaji
mwanafunzi anaweza kujua maana ya uraia
na umuhimu wa uraia.

Kielelezo Na. 8.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 8

Katika Kielelezo Na. 8.2 mtahiniwa alijaribu (a) kueleza lengo mahususi la ufundishaji wa dhana ya Uraia na (b) kueleza mfano wa maoni ya mwalimu kwenye andalio la somo la Uraia badala ya kueleza dhana ya vitendo vya ufundishaji na ujifunzaji, hivyo alipata alama 0.

### 2.1.9 Swali la 9: Utamaduni Wetu


Swali lilimtaka mtahiniwa kuonesha umuhimu wa mwalimu tarajali kuchunga mwenendo wake anapokuwa katika mazoezi ya ufundishaji wa muda mrefu kwa kutoa hoja nne. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa asilimia 98.1 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na. 9.




**Chati Na.** *9: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 9*

Chati Na. 9 inaonesha kuwa, asilimia 1.9 ya watahiniwa waliofanya swali hili, walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5; asilimia 4 walipata alama 2 na asilimia 94.1 walipata kuanzia alama 3 hadi 4.


Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa wengi (94.1%) walipata alama 3 hadi 4 kwa kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ndogo ya Maandalizi ya Ufundishaji wa Muda Mrefu. Watahiniwa hao walielewa matakwa ya swali hivyo walieleza umuhimu wa mwalimu tarajali kuchunga mwenendo wake anapokuwa katika mazoezi ya ufundishaji wa muda mrefu. Baadhi ya majibu sahihi ya watahiniwa yalikuwa ni; *huendeleza mahusiano mazuri na wenyeji, hujiongezea uzoefu na utaalamu katika kazi yake, huongeza heshima binafsi na hufanya kuaminiwa, kujifunza mambo mapya na kupewa ushirikiano unaofaa na wenyeji* na *hudumisha sifa nzuri ya chuo anachotoka.* Kielelezo Na. 9.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetoa majibu sahihi katika swali hili.


9 (i) Husaidia kujijengea heshima yeye kama mwalimu tarajali katika jamii yake.
(ii) Huweza kumsaidia kuepuka migogoro mwalimu tarajali ambayo ingeweza kutokea.
(iii) Huweza kupelekea walimu wenyeji kumpenda mwalimu tarajali na kuweza kumuomba arudi baada ya kumaliza mafunzo ili akaweze kuwasaidia katika kufundisha watoto shuleni.
(iv) Huweza kumpelekea mwalimu tarajali kuaminiwa na jamii.

Kielelezo Na. 9.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 9

Aidha, asilimia 4 ya watahiniwa walipata ufaulu wa wastani ambapo baadhi yao walielezea majibu pungufu na wengine walirudia jibu zaidi ya mara moja au walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Mtahiniwa mmoja kwa mfano alichanganya hoja zisizo sahihi kwenye majibu yake kwa kuandika; *mwalimu anaweza kupoteza ajira* na *mwalimu anaweza kukosa alama*.

Watahiniwa wachache (1.9%) waliopata ufaulu hafifu katika swali hili baadhi yao (1%) walitoa hoja pungufu ya mbili au walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi, hivyo walipata alama 1 au 1.5. Watahiniwa wengine (0.9%) waliopata alama 0, baadhi yao hawakuelewa matakwa ya swali na wengine hawakuwa na maarifa kuhusu dhana husika. Mtahiniwa mmoja kwa mfano alikosa swali hili kwa kuandika majibu kama; *mcheshi*, *mpole* na *mnyenyekevu*; bila kutoa maelezo yoyote. Kielelezo Na. 9.2 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kuonesha kwa usahihi umuhimu wa mwalimu tarajali kuchunga mwenendo wake anapokuwa katika mazoezi ya ufundishaji wa muda mrefu.


9. i. kufahamu haki na usawa wa kijinsia kwa wanafunzi: kuwapa wanafunzi wote haki sawa bila kubaguwa msichana au mvulana au kuwapa upendeleo wowote wa alama kwa jinsia fulani

ii Demokrasia
kuwapa fursa ya wanafunzi kujitetea au kuongea na kujieleza shida zinazowakuta zinazowakabili akiwa nyumbani kama uchelewaji, kutokahudhuria

iii/ Utawala wa sheria
Kutokuwepo kwa sheria ambayo inakuwa inakandamiza kwa upande mmoja wa jinsia au mtu yeyote ambaye ana makosa


iv/ kupiga kura
kutotoa kura au kupokea kura yeyote kutoka kwa wanafunzi au kutoa kura kwa ajili ya ngono uzembe na Wanafunzi

Kielelezo Na. 9.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 9

Katika Kielelezo Na. 9.2 mtahiniwa alihusisha dhana mbalimbali zinazofundishwa kwenye somo la Uraia kama; *demokrasia*, *haki* na *usawa wa kijinsia*, *kupiga kura* na *utawala wa sheria* na kiini cha swali badala ya kueleza umuhimu wa mwalimu tarajali kuchunga mwenendo wake anapokuwa katika mazoezi ya ufundishaji ya muda mrefu, hivyo alipata alama 0.

### 2.1.10 Swali la 10: Upimaji na Tathmini


Swali lilimtaka mtahiniwa kuonesha ni kwa namna gani tathmini endelezi hutofautiana na tathmini tatuzi. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa asilimia 97.4 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na. 10.




**Chati Na. 10:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 10*

Chati Na. 10 inaonesha kuwa, asilimia 2.6 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata kuanzia alama 0 hadi 1; asilimia 3.8 walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na asilimia 93.6 walipata kuanzia alama 3 hadi 4.

Uchambuzi unaonesha kuwa, watahiniwa wengi (93.6%) waliweza kutofautisha kati ya tathmini endelezi na tathmini tatuzi na hivyo walipata alama tatu hadi nne kutokana na usahihi wa maelezo ya kila mmoja. Watahiniwa hao, walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ndogo ya Tathmini Katika Somo la Uraia na walielewa matakwa ya swali. Majibu sahihi katika swali hili yalikuwa kama; *tathmini endelezi ni ile inayofanyika wakati wote katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji katika somo ili kufuatilia kuona kama ujuzi unaokusudiwa kwa mwanafunzi anaupata kikamilifu* wakati *tathmini tatuzi ni ile inayotafuta chanzo cha tatizo kilichobainishwa katika tathimini endelezi na kushindwa kupatiwa ufumbuzi*. Kielelezo Na. 10.1 ni mfano wa jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri.




10. Tathmini endelezi; ni aina ya tathmini ambayo hufanywa
mara kwa mara ndani na nje ya darasa mfano mazoezi kila ba
ada ya kipindi, majaribio ya wiki, mwezi na kazi za kufanya
nyumbani kwa lengo la kujua maendeleo ya wanafunzi lakini
Tathmini tatuzi, hufanyika kwa lengo la kurekebisha tati
zo au changamoto iliyo jitokeza kwa lengo la kuboresha au
kuinua maendeleo ya wanafunzi.

Kielelezo Na. 10.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 10

Asilimia 3.8 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 kwa kuwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana husika. Baadhi ya watahiniwa hao waliandika upande mmoja wa swali na wengine walieleza tofauti dhaifu na hivyo walipata alama za wastani.

Watahiniwa wachache (2.6%) walipata alama 0 hadi 1 ambapo baadhi yao (0.7%) walikuwa na maarifa hafifu kuhusu dhana husika na hivyo walitoa majibu dhaifu au kuandika upande mmoja wa swali uliosababisha kupata alama 1. Mtahiniwa mmoja kwa mfano aliandika; *tathmini endelezi hufanyika mara kwa mara*; na alishindwa kujibu upande wa pili wa swali, hivyo alipata alama pungufu. Watahiniwa wengine (1.9%) hawakuelewa matakwa ya swali au hawakuwa na maarifa kuhusu dhana husika. Mtahiniwa mmoja kwa mfano aliandika majibu yasiyo sahihi kama; *tathmini endelezi ni tathmini ambayo hupimwa mwishoni mwa mada ndogo* wakati *tathmini tatuzi hupimwa baada ya mada kuu kuisha*. Kielelezo Na. 10.2 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kuonesha kwa usahihi ni kwa namna gani tathmini endelezi hutofautiana na tathmini tatuzi.



| | | |
|---|---|---|
| 10. | tathimini endeleu ni aina ya tathimini ambaya inatumiwa na watu wengi. | tathimini tatuzi ni aina ya tathimini ambayo inatumiwa na watu wachache. |

Kielelezo Na. 10.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 10


Katika Kielelezo Na.10.2 mtahiniwa aliandika majibu ya kubuni ya kutofautisha dhana hizo kama; *tathmini endelezi inatumiwa na watu wengi* wakati *tathmini tatuzi inatumiwa na watu wachache* bila kutoa maelezo ya kina badala ya kutoa ufafanuzi sahihi wa tathimini endelezi na tathimini tatuzi, hivyo alipata alama 0.

### 2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha (Taaluma)

Ufaulu wa watahiniwa katika sehemu hii uligawanyika katika makundi matatu ambapo, mtahiniwa alikuwa na ufaulu hafifu endapo alipata kuanzia alama 0 hadi 5.5, ufaulu wa wastani endapo alipata kuanzia alama 6 hadi 10 na alikuwa na ufaulu mzuri endapo alipata kuanzia alama 10.5 hadi 15.

### 2.1.11 Swali la 11: Dola

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kuchambua vikwazo vitano dhidi ya utawala wa kidemokrasia katika nchi. Kwa ujumla ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa asilimia 92 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 6 hadi 14.5 kama inavyoonekaa katika Chati Na.11.




**Chati Na. 11:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 11*

Chati Na. 11 inaonesha kuwa, asilimia 8 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata kuanzia alama 0 hadi 5.5; asilimia 36.8 walipata kuanzia alama 6 hadi 10 na asilimia 55.2 walipata kuanzia alama 10.5 hadi 14.5.


Takwimu zinaonesha kuwa asilimia 55.2 ya watahiniwa walipata ufaulu mzuri katika swali hili. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada ndogo ya Utawala wa Kidemokrasia na walielewa matakwa ya swali. Mfano wa majibu sahihi waliyotoa ni; *ukiukwaji wa sheria*, *kutowajibika kwa viongozi*, *rushwa*, *ukiukwaji wa misingi ya haki za binadamu*, *kutokuwa na ukweli na uwazi* na *kutokuwepo kwa uhuru wa vyombo vya habari*. Wengi wa watahiniwa hao walianza na utangulizi uliojitosheleza na walitoa maelezo sahihi ya kutetea hoja zao. Tofauti ya alama kati ya watahiniwa ilitokana na maelezo ya kila mmoja. Kielelezo Na. 11.1 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyechambua kwa usahihi vikwazo vitano dhidi ya utawala wa kidemokrasia katika nchi.

11. Utawala wa kidemokrasia huu ni utawala ambao viongozi wake huongoza kwa kuzingatia misingi ya kidemokrasia ambayo ni uwazi, uwajibikaji, uadilifu, utawala wa sheria, uzingatiaji wa haki za binadamu na mambo mengine mengi. yafuatayo ni mambo yanayokwamisha utawala wa kidemokrasia nchini

Kuwepo kwa vitendo vya rushwa nchini; katika nchi yetu kuna tatizo kubwa sana la ukwamisi kwa vile ndio vya rushwa kwa baadhi ya viongozi wa serikali, jambo hili huwa kikwazo kikubwa cha kuwa na demokrasia au uongozi wa kidemokrasia kwani uongozi wa kidemokrasia huwa hauhusishi vitendo vya rushwa.

Kutokuwepo na uwazi wa baadhi ya mambo yanayoendelea nchini mfano nchini Tanzania kumetokea tatizo la kuugua kwa mtu aliyekuwa wa raisi wa awamu ya Tano ya Tanzania lakini taarifa za kuugua kwake zikafichwa na kuachiwa kutangazwa kwahiyo vitendo kama hivyo na vitendo vingine hufanya kusiwe na uongozi wa kidemokrasia katika nchi.

Kutoajibika ipasavyo kwa baadhi ya viongozi; kuajibika ni kitendo cha kutekeleza majukumu yako kwa wakati kama inavyotakiwa. Baadhi ya viongozi nchi hawatekelezi majukumu yao kwa



Wakati unaotakiwa hivyo kutokana na hili husababisha sifa ya kuwa na uongozi wa kidemokrasia kukosa nchini.

Kutokuwepo na mgawanyo wa Madaraka; ili kuwa na uongozi wa kidemokrasia nchini sharti kuwepo na mgawanyo sahihi wa madaraka. katika nchi nyingi, viongozi wakuu wa nchi huingilia madaraka badala ya viongozi wa sekta husika mfano Rais kusimamia uchimbaji wa madini badala ya kusimamia waziri wa madini na viongozi wengine wanaohusika.

Kutokuwepo kwa utawala wa sheria nchini; utawala wa sheria huu ni utawala ambao huzingatia sheria ambayo mtu yeyote mwenye kosa huadhibiwa kulingana na kosa lake bila ya kuonewa wala kupendelewa. nchi nyingi huwaonea hazifuati utawala wa sheria ambapo viongozi wa nchi wanapotenda makosa, hawaadhibiwi sawa na anavyo adhibiwa raia wa kawaida kwa hivyo hii husababisha kutokuwepo kwa uongozi wa kidemokrasia nchini


Yote kwa yote utawala wa kidemokrasia katika nchi hujengwa na kuwepo kwa usawa, uwajibikaji, uadilifu, uzingatiaji wa haki za binadamu, mgawanyo wa madaraka na kuwepo kwa vyama vingi vya siasa katika nchi.

Kielelezo Na. 11.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 11

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa asilimia 36.8 ya watahiniwa waliopata kuanzia alama 6 hadi 10 katika swali hili, hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya Utawala wa Kidemokrasia. Hii ni kwasababu baadhi ya

watahiniwa walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Mtahiniwa mmoja kwa mfano aliandika majibu yasiyo sahihi kama; *milipuko ya magonjwa*, *ukosefu wa miundo mbinu* na *kuporomoka kwa uchumi*. Watahiniwa wengine katika kundi hili walitoa majibu machache na ufafanuzi usiotosheleza matakwa ya swali, hivyo walifaulu kwa kiwango cha wastani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache (8%) waliopata kuanzia alama 0 hadi 5.5, baadhi yao (7.7%) walikuwa na maarifa hafifu kuhusu dhana iliyoulizwa, hivyo kutoa majibu pungufu au kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi yalisababisha kupata alama za chini. Wengine (0.3%) katika kundi hili waliopata alama 0, baadhi yao hawakuwa na maarifa kabisa kuhusu dhana ya Utawala wa Kidemokrasia na wengine hawakuelewa matakwa ya swali hivyo kutoa majibu kinyume na dhana iliyoulizwa. Mtahiniwa mmoja kwa mfano alichanganya dhana mbalimbali zilizopo kwenye somo la Uraia kwa kuandika dhana kama; *sera, siasa, mfumo wa vyama vingi* na *kubadilika kwa itikadi,* ambazo hazikuwa sahihi. Mtahiniwa mwingine aliandika majibu yasiyo sahihi kwa hoja kama; *viongozi bora*, *uchaguzi wa haki*, *maendeleo ya nchi*, bila kutoa maelezo yenye kuziunganisha hoja hizo na vikwazo dhidi ya utawala wa Kidemokrasia kwenye nchi. Kielelezo Na. 11.2 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyeshindwa swali hili.


r/- demokrasia, ni kikundi ch
a watu kinachotawaliwa
na watu.
Vifuatazo ni vikwazo dhi
di ya utawala wa kide
mokrasia katika nchi.
husaidia kutokomeza
uizi, katika demokrasia
hii uuizi ukitokomezwa kati
ka nchi watu wanaweza
wakakaa kwa utulivu na
kuweza kujitawala wao
wenyewe.
husaidia kutokomeza uja
mbazi, katika nchi hii uja
kuwengu ni jambazi kutoka
na na maringira wana
ya ishi wao wenyewe na
kuweza kwa kutokomeza
vitu kama hivo na ku
weza kutatua tatizo katika nchi
husaidia kutoko meza
ugonvi, katika nchi
ya kidemokrasia ukiteka
kuishi kiusalama unate
kwa utokomeze vitu ka
ma hivo na kuweza kuwa
na ushirikiano kati ya
jamii moja na nyingine
husaidia kutokomeza usala
na katika nchi, mwana demo
krasia nanatakiwa ajilinde
yeye mwenye na aweze
kujipenda bila yeye kutoka kw
a jamii nyingine na kuweza
kujisaidia mwenyewe.
husaidia kujenga wam
lofu, mtu unapokuwa mwami
mifu katika nchi unatetki
wa kuwa karibu sana na
demokrasia ya nchi na ku
weza. kujiongoza wewe
na kuweza kutetea nchi
yako
Hitimisho, hivo ndivyo vik
wazo vinavyo tokea katika
nchi mfano uuizi. kuko
mesha uuizi katika nchi


Kielelezo Na. 11.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 11

Kielelezo Na. 11.2 kinaonesha kuwa mtahiniwa hakuwa na maarifa kuhusu dhana ya Utawala wa Kidemokrasia na hivyo alitoa majibu ambayo

hayakuwa na uhusiano na swali kwa hoja kama; *husaidia kutokomeza wizi*, *ujambazi* na *ugomvi* badala ya kuchambua vikwazo dhidi ya Utawala wa Kidemokrasia katika nchi.

### 2.1.12 Swali la 12: Utamaduni Wetu

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kufikiria endapo ameteuliwa kumuwakilisha Mkuu wake wa Shule katika kikao cha maadili katika Wilaya yao, afafanue hoja tano atakazozitoa kama njia zinazoweza kutumika katika kudumisha maadili mema kwa jamii. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa asilimia 99.5 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 6 hadi 15 kama inavyoonekana katika Chati Na.12.





**Chati Na. 12:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 12*

Chati Na. 12 inaonesha kuwa, asilimia 0.5 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata kuanzia alama 0 hadi 5; asilimia 13.9 walipata kuanzia alama 6 hadi 10 na asilimia 85.6 walipata kuanzia alama 10.5 hadi 15.

Watahiniwa wengi (85.7%) walipata alama za juu kwa kuwa walitoa utangulizi uliojitosheleza, ufafanuzi mzuri wa njia zinazoweza kutumika kudumisha maadili mema katika jamii na hitimisho lenye uhusiano na swali. Tofauti ya alama kati yao ilitokana na usahihi wa hoja na maelezo yaliyotolewa na kila mmoja. Ufaulu mzuri wa watahiniwa hao ni kielelezo kuwa walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada ya Utamaduni Wetu na walielewa matakwa ya swali.  Baadhi ya majibu sahihi yaliyotolewa katika

swali hili ni; *familia kufundisha maadili kwa watoto, walimu kusimamia maadili mema kwa wanafunzi wote (kuandaa vipindi vya maadili), jamii kusimamia maadili ya watu wote, vikundi vya dini kuhakikisha jamii inakuwa na maadili mema* na *vyombo vya habari vinaweza kutumika kurithisha maadili mema kwa jamii*. Kielelezo Na. 12.1 ni mfano wa jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.



12. Maadili mema ni tabia mienendo, ma
lezi mema ambayo mtu huwa nayo yanayomw
onga kuishi katika jamii bila migogoro au ubu
mbufu wowote mfano kuvaa vizuri mavazi ya
nayo ~~ft~~ stili mwili, namna ya kuongea / kuwasiliana.
Zifuatazo ni njia zinazoweza kutumika kati
ka kudumisha maadili mema kwa jamii.
Kutoa elimu kwa vijana kuhusiana na
maadili mema. Hii husaidia vijana au jamii
kuweza kujiepusha na vitendo vya kiovu m
fano wizi, mapenzi pamoja matumizi ya ma
dawa ya kulevya.
Pia kutungwa kwa sheria pamoja na ku
toa sera nzuri inayohimiza kukuza maadili
kwa ~~ja~~ jamii; Hii itasaidia na kufanya kila
mtu au mwanajamii kuepuka kujiepusha ~~na~~
na maovu hayo huweza kuchangia kuwepo
kwa uajibikaji.

Kuzuia mitandao ya kijamii inayohu
sisha matendo ya kiovu; Hii itasaidia kwa
sababu mitandao ya kijamii hufunya watu wa
shawishi na maovu mfano mikanda ya X hu
pelekea kuchochea mahusiano ya kimapenzi
pamoja na kujichichora tatuu.
Pia kuendeleza mila na destuni zina
zo dumisha maadili mema: Hii husaidia
mafunzo kwa vijana katika jamii na kuwa
nya kuadilika mfano namna ya uvaaji wa
mavazi kusalimiana kuongea "Kuzuia
jamii kuepuka kuig
na mila na destuni za kigeni zinazochang
ia kuporomoka kwa maadili. Mfano namna
ya kunyoa, kuvaa visketi fupi pamoja na mo
do.
Kutoa ushauri wa kuhimiza watu ku
shiriki katika vipindi vya dini: Hii husai
dia kujenga maadili mema kutokana na
mafunzo ya kiimani na kuweka kuwa na
hofu katika kutenda maovu mfano hofu ya
kuzimu, kaburi, kutukana na kadharau
hufunya mtu aogope kwa mungu alamchona
Hivyo basi ili kudumisha maadili
mema haina budi kila jamii kuajibika na
kuunda vikundi vya ushauri na vya kidini
ili kuendeleza kudumisha maadili mema

Kielelezo Na. 12.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 12

Takwimu zinaonesha kuwa, asilimia 13.9 ya watahiniwa waliopata alama za wastani katika swali hili, baadhi yao walitoa majibu pungufu na ufafanuzi usiotosheleza matakwa ya swali na wengine walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Mtahiniwa mmoja kwa mfano alichanganya majibu ambayo yalikuwa dhaifu kwa hoja kama; *ni marufuku kunywa pombe kali, ni marufuku kuvaa nguo za kubana* na *ni marufuku kujihusisha na mahusiano*

bila kutoa maelezo ya kina kuhusu hoja hizo hivyo walipata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache (0.5%) waliopata alama hafifu katika swali hili, baadhi yao (0.4%) walikuwa na maarifa hafifu kuhusu dhana iliyoulizwa, hivyo walitoa majibu dhaifu yaliyosababisha kupata alama hafifu (2 – 5). Watahiniwa waliobakia (0.1%) katika kundi hili hawakuelewa matakwa ya swali, hivyo walitoa majibu tofauti na matakwa ya dhana iliyoulizwa. Mtahiniwa mmoja kwa mfano alifafanua sababu za mmomonyoko wa maadili kwa vijana katika jamii kwa hoja kama; *mitandao ya kijamii*, *makundi hatarishi* na *tamaa za maisha*. Kielelezo Na. 12.2 ni mfano wa jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kutoa njia tano zinazoweza kutumika katika kudumisha maadili mema kwenye jamii kwa usahihi.

12 Mwalimu mkuu, ni mtu ambae anaweza kuongoza shule


Zifuatazo ni sifa za mwalimu mkuu.

Awe na uwezo wa kusimama mbele ya watu, mwalimu anatakiwa awe ze kusimama mbele ya watu na kuweza kuongea mbele ya watu na kuweza kujibu maswali anayo ulizwa na watu.

Awe mcheshi, mwalimu mkuu anatakiwa awe mcheshi mbele ya watu na kuweza kuwajali watu na kuwasikiliza watu ambao wapo kwenye mkutano huo na kuweza kuwa sikiliza

Awe na haiba ya mwaalimu, mwalimu mkuu anatakiwa awe smati kwenye mavazi ya uhaiba ya mwalimu na kuweza kujibu maswali atakayo ulizwa na watu waliopo kwenye kikao hicho

Awe na uwezo wa kujiamini, mwalimu mkuu anatakiwa awe anajiamini kutoka mbele ya watu na



kuweza kuulizwa masuala na watu walioko ndani ya jengo hilo
awe na roho ya huruma mwalimu mkuu anatakiwa awe na moyo wa huruma kwa viongozi wengine.
Hitimisho, mwalimu mkuu anatakiwa awe na sifa kama hizo, na kuweza na kuweza kuwaongoza wengine"

Kielelezo Na. 12.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 12

Katika Kielelezo Na.12.2 mtahiniwa alieleza sifa za mwalimu mkuu kwa kutoa hoja kama; *awe na uwezo wa kusimama mbele za watu, awe mcheshi, awe na haiba ya ualimu, aweze kujiamini* na *awe na huruma* badala ya kueleza njia zinazoweza kutumika katika kudumisha maadili mema kwenye jamii hivyo alipata alama 0.

## 2.1.13 Swali la 13: Uhusiano wa Kimataifa

Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa kutumia hoja sita namna ambavyo Msingi wa Kutofungamana na Upande Wowote unavyoinufaisha Tanzania katika utekelezaji wa sera yake ya Mambo ya Nje. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa asilimia 88.7 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 6 hadi 14 kama inavyoonekana katika Chati Na. 13.





**Chati Na. 13:** *Ufaulu wa watahiniwa* katika swali la 13

Chati Na. 13 inaonesha kuwa, asilimia 11.3 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata kuanzia alama 0 hadi 5.5; asilimia 55.6 walipata kuanzia alama 6 hadi 10 na asilimia 33.1 walipata kuanzia alama 10.5 hadi 14.

Takwimu zinaonesha kuwa nusu ya watahiniwa (55.6%) waliofanya swali hili, walipata alama za wastani. Baadhi yao waliweza kutoa utangulizi sahihi lakini walishindwa kufafanua majibu yao vizuri. Wengine kati yao walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Mtahiniwa mmoja kwa mfano mbali na kushindwa kutoa utangulizi na hitimisho lenye kujitosheleza, alichanganya na majibu yasiyo sahihi kwenye insha yake kwa hoja kama; *husaidia kupata viongozi bora* na *kusaidia kupunguza vitendo viovu* bila kutoa maelezo fasaha, hivyo alipata alama za wastani.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, asilimia 33.1 ya watahiniwa waliopata kuanzia alama 10.5 hadi 14 walielewa matakwa ya swali na hivyo walifafanua kwa kina namna Msingi wa Kutofungamana na Upande Wowote unavyoinufaisha Tanzania katika utekelezaji wa sera yake ya Mambo ya Nje. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kina kuhusu mada ndogo ya Maeneo ya Mahusiano ya Kimataifa. Baadhi ya majibu sahihi katika swali hili ni kama yafuatayo: *kukataa kuchaguliwa marafiki washirika na mataifa mengine, kupitia uhusiano wa kidiplomasia na nchi nyingine kwa kuzingatia misingi ya kutofungamana na upande wowote imesaidia Tanzania kujitangaza kijamii, kiuchumi na kiutamaduni*


*katika jumuiya mbalimbali, kulinda uhuru wa nchi yetu, kulinda mahusiano na nchi marafiki, kufungua fursa mbalimbali kwa wingi kwa raia wake* na *kuepuka migogoro na migongano ya mataifa mengine*. Kielelezo Na. 13.1 ni mfano wa sehemu ya jibu la mtahiniwa aliyepata ufaulu mzuri katika swali hili.


13 Tanzania imefanikiwa kutangaza sera zake za utalii na kupata watalii wengi kutoka mataifa ya nje, mfano Norway, Denmark, Sweden, Marekani, Uingereza na kwingineko.
Tanzania imeweza kunufaika na masuala ya ulinzi na usalama, kutokana na msingi huu wa kutokufungamana na upande wowote umeiwezesha Tanzania kupata mafunzo ya kijeshi kwa wanajeshi wake nje ya nchi mfano CUBA lakini pia ni moja ya nchi mwanachama wa UNITED NATIONAL (UN) ambapo wanajeshi wa Tanzania wameweza kwenda nchi mbalimbali za Afrika kama Congo DRC Central Africa na nchi zingine zenye machafuko.
Tanzania imefanikiwa kueleza masoko ya bidhaa zake nje ya nchi, kutokana na kutokufungamana na upande wowote wa sera za kidunia Tanzania imepanua sana masoko yake mfano: kuuza mazao nje ya nchi kwenye soko huria na madini.
Tanzania imefanikiwa kupata wawekezaji wengi kutoka nje ya nchi, kulingana na sera ya mambo ya nje Tanzania imeweza kuwavutia wawekezaji wengi kutoka mataifa mbalimbali Ulaya, Asia, Amerika na Australia. mfano makampuni ya Sheli ya TOTAL OIL, kampuni ya madini ACACIA hivyo utekelezaji wa sera ya mambo ya nje umeweza kufanikiwa kwa kiasi kikubwa

Kielelezo Na. 13.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 13

Katika Kielelezo Na. 13 mtahiniwa alieleza namna Msingi wa Kutofungamana na Upande Wowote unavyoinufaisha Tanzania katika utekelezaji wa sera yake ya Mambo ya Nje. Hata hivyo, mtahiniwa hakupata alama zote 15 kutokana na kiwango cha ufasaha katika baadhi ya maelezo yake.

Kwa upande mwingine, asilimia 11.3 ya watahiniwa walipata ufaulu hafifu. Wengi kati ya watahiniwa hao (11.2%) walikuwa na maarifa hafifu kuhusu dhana iliyoulizwa hivyo walishindwa kutoa maelezo fasaha kutetea hoja zao na wengine walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Mtahiniwa mmoja kwa mfano alichanganya katika majibu yake hoja ambazo si sahihi kama; *kusaidia kuzuia wimbi kubwa la ujambazi na wizi*, *husaidia kukwepa magonjwa mbalimbali* na *husaidia kukuza tamaduni za nchi mbalimbali*. Mtahiniwa mmoja (0.1%) aliyebakia alipata alama 0. Mtahiniwa huyo hakuelewa matakwa ya swali na hivyo kutoa majibu kinyume na dhana iliyoulizwa kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 13.2.



13 Sera ni dira ya nchi katika jambo fulani - Tanzania huwa na sera nyingi ambazo hutekeleza katika mambo yake ya nje lakini sera hizi huwa huweza kufungamana baina ya nchi na nchi Lakini pia huwa za kutofungamana na nchi yoyote. Tanzania hunufaika katika kutekeleza misingi yake na kutekeleza misingi hiyo kwa kutofungamana. Yafuatayo ni mambo ambayo Tanzania hunufaika katika utekelezaji wa sera zao na mambo ya nje.

Husaidia kutokuja kwa tamaduni za kigeni; hii ni faida ambayo Tanzania wanaipata katika utekelezaji wa sera yake ya mambo ya nje kwani kuja kwa tamaduni za kigeni huwa na madhara makubwa kwa nchi husababisha mila na desturi za tanzania kutoweka au kupotea.

Huimarisha mila na desturi za ~~kit~~ Kitanzania; katika utekelezaji huo wa sera za tanzania hunafaika na kufanya Tanzania kuwa imara na kuendeleza mila na desturi zao za Kitanzania kwani misingi huo unaakuwa haufungamani na upande mwingi na wowote.

Husaidia kupata viongozi walio bora; hii ni mambo ambalo Tanzania hunufaika kupitia misingi isiyo fungamana kwani hutuwezesha Tanzania kupata viongozi walio bora ambao hutasaidia katika kuleta maendeleo katika nchi ya Tanzania.

Kielelezo Na. 13.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 13


Katika Kielelezo Na. 13.2 mtahiniwa alidhani kuwa Msingi wa Kutofungama na Upande Wowote ni sera inayoitenga Tanzania na Mataifa mengine na hivyo kutoa majibu kama; *husaidia kutokuja kwa tamaduni za kigeni* na *huimarisha mila na desturi za Kitanzania* badala ya kueleza namna ambavyo msingi huo unavyoinufaisha Tanzania katika utekelezaji wa sera yake ya Mambo ya Nje.

## 2.3 SEHEMU C: Maswali ya Insha (Utaalamu)

Ufaulu wa watahiniwa katika sehemu hii uligawanyika katika makundi matatu ambapo, mtahiniwa alikuwa na ufaulu hafifu endapo alipata kuanzia alama 0 hadi 5.5; ufaulu wa wastani endapo alipata kuanzia alama 6 hadi 10 na alikuwa na ufaulu mzuri endapo alipata kuanzia alama 10.5 hadi 15.

### 2.1.14 Swali la 14: Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la Uraia

Swali lilimtaka mtahiniwa kwa kutoa hoja tano kutetea kauli ya kuwa “Stadi ya kutafuta, kuchambua na kutumia taarifa ni muhimu kwa mtu kuwa raia mwema”. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa asilimia 76.6 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 6 hadi 14.5 kama inavyoonekana katika Chati Na. 14.





**Chati Na. 14:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 14*

Chati Na. 14 inaonesha kuwa, asilimia 23.4 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata kuanzia alama 0 hadi 5.5; asilimia 55.3 walipata kuanzia alama 6 hadi 10 na asilimia 21.3 walipata kuanzia alama 10.5 hadi 14.5.

Uchambuzi unaonesha kuwa, nusu ya watahiniwa (55.3%) walipata alama za wastani katika swali hili, kwasababu walikuwa na mapungufu kadhaa katika majibu yao kama; maelezo yasiyojitosheleza kutetea hoja, idadi ndogo ya majibu kinyume na matakwa ya swali, utangulizi na hitimisho lisiloendana na swali na wengine walichanganya majibu sahihi na yasiyo

sahihi. Mtahiniwa mmoja kwa mfano alichanganya kwenye majibu yake hoja zisizo sahihi kama; *huondoa dhana ya mila potofu katika jamii*, *husaidia swala la ajira* na *hurejesha furaha na matumaini*, hivyo alipata alama za wastani.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, asilimia 23.4 ya watahiniwa waliopata alama 0 hadi 5.5, baadhi yao (23.1%) walikuwa na maarifa hafifu kuhusu dhana husika na hivyo waliweza kuandika angalau utangulizi na hoja chache ambazo walishindwa kuzitetea, hivyo kupata alama za chini. Wengine (0.3%) waliopata alama 0, hawakuelewa matakwa ya swali na hivyo kutoa majibu tofauti na dhana iliyoulizwa. Mtahiniwa mmoja kwa mfano alifafanua umuhimu wa kutumia taarifa za kiutafiti kwa hoja kama; *kuondoa dhana ya mila potofu, husaidia kuchochea maendeleo katika jamii, husaidia kubaini chanzo cha tatizo na kulitafutia suluhu* na *husaidia swala la kujiajiri kwa mtafiti*. Mtahiniwa mwingine, alifafanua mchango wa raia mwema kwenye jamii kwa hoja kama; *husaidia kubaini wahalifu katika jamii*, *husaidia watu katika jamii* na *huweza kubaini mambo hatarishi katika jamii*. Kielelezo Na. 14.1 ni mfano wa sehemu ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.


14. Raia ni mtu mwenye haki kisheria za kuwa na uraia wa nchi fulani kwa kuzaliwa nasaba au kwa kuomba.

Zifuatazo ni sifa za kuwa raia mwema katika nchi husika.

Kulipa kodi kwa serikali yake, raia mwema hulipa kodi halali bila kukwepa ambayo huongeza pato la taifa na serikali kutoa huduma za kijamii mfano ujenzi wa barabara, kusambaza maji kujenga vituo vya afya na kusambaza ~~maji~~ umeme.

Hulinda mali ya umma, mfano mabomba ya maji, transifoma ili aendelee kupata huduma na kuiepushia serikali gharama zisizo za msingi.

Anakubaliana na maoni ya walio wengi, mfano katika mikutano ya hadhara, kukubaliana na matokeo ya uchaguzi, kwa maslahi ya maendeleo ya nchi yake.

Anahudhuria shughuli zote za kimaendeleo, mfano katika ujenzi wa madarasa na hospitali, hivyo kuendelea kuikuza nchi yake katika nyanja zote bila shida yoyote.


Anatii sheria bila shuruti, mfano kutokuiba, kutojilimbikizia mali kinyume cha sheria, hivyo kuifanya nchi yake kuwa na amani na utulivu nchi kuendelea.

Kielelezo Na. 14.1: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 14

Katika Kielelezo Na. 14.1 mtahiniwa alifafanua sifa mbalimbali za raia mwema katika nchi badala ya kueleza umuhimu wa stadi ya kutafuta, kuchambua na kutumia taarifa kwa mtu kuwa raia mwema.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache (21.3%) walipata ufaulu mzuri kwa kuwa walielewa matakwa ya swali. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu kipengele cha Ufundishaji unaozingatia ujenzi wa stadi na ujuzi wa kiraia. Majibu sahihi ya swali hili yalikuwa ni; *stadi hii inafundisha mbinu za kukusanya taarifa, kufanya tathimini ya vyanzo vya taarifa na kujitegemea katika kukusanya taarifa, pia stadi hii ni muhimu kwa sababu inafundisha jinsi ya kuchambua taarifa, husaidia kupanga*

*taarifa zilizokusanywa na hatimaye kupata taarifa sahihi, husaidia kupanga taarifa zilizokusanywa na kuondoa utata, husaidia kuhifadhi taarifa kwa matumizi ya baadae* na *husaidia mtu kutumia taarifa alizotafuta katika maisha yake*. Kielelezo Na. 14.2 ni mfano wa sehemu ya jibu la mtahiniwa aliyepata ufaulu mzuri katika swali hili.


14. Rai mwema ni mtu yeyote ambaye ni mwaminifu
kwa nchi yake na analinda na kutuma sheria za nchi. Stadi
ya kutafuta, kuchambua na kutumia taarifa ni muhimu kati
ka kumjenga mtu kuwa rai mwema. Zifuatazo ni hoja kuone
sha jinsi gani stadi hii ni muhimu kwa raia mwema;
kwanza itamjengea uwezo wa kutafuta taarifa sahihi;
Raia mwema ni yule anayetafuta taarifa kwa usahihi na
kwa kutumia vyombo sahihi na sio maneno ya mitandaoni
mfano kupitia Televisheni na redio ya taifa hapa ndipo
rai mwema anaweza kupata taarifa sahihi.
kuwa na uwezo wa kuchambua taarifa; Taarifa
mbalimbali huweza kutolewa kupitia redio, Televisheni na
mitandaoni baadhi yao zikiwa sahihi na nyingine zikiwa
za uongo. Sasa stadi hii humpatia uwezo raia mwema kujua

14. Kipi sahihi na kipi si sahihi kwa kuzichambua.
Itampatia uwezo wa kutumia taarifa kwa usahihi;
Raia mwema ni yule anaezingatia maagizo ya Serikali yake
na kutii bila shuruti. Mfano taarifa imetolewa ikiwaomba watu
wote kusimama wimbo wimbo wa taifa unapoimbwa basi taarif
a hiyo lazima aitumie kutii sheria.
Stadi hii humuongezea uwezo wa kufikiri kabla ya
kutenda; Zipo taarifa ambazo hutolewa kwaajili ya kuleta
bisha machafuko sasa endapo ilitamfikia raia mwema ambaye
amepata stadi hii kwanza lazima afikirie ndipo aamue. Mfano
waanzilishi wa maandamano muda mwingi huwa hawafikirii.
Itampatia kutoshiriki katika matendo ya uvunjifu
wa amani; Baada ya kuwa amepata stadi hii na kuielewa
kikamilifu basi itamsaidia mtu kuwa na hofu ya uzalendo na
kufanya mambo kwa faida mfano kusema serikali mitandaoni raia
mwema hawezi kupoteza muda wake kuchangia mada.
Stadi ya kutafuta, kuchambua na kutumia taarifa
ni muhimu kwa mtu kuwa raia mwema kama hoja zilivyoelezwa
hapo juu. Hivyo basi serikali isisitize utoaji wa stadi hii ili
kuwezesha kupata raia ambao ni wema.


Kielelezo Na. 14.2: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 14

Katika Kielelezo Na. 14.2 mtahiniwa alifafanua umuhimu wa stadi ya kutafuta, kuchambua na kutumia taarifa kwa mtu kuwa raia mwema. Hata hivyo, mtahiniwa hakupata alama zote 15 kutokana na mapungufu madogo kwenye ufafanuzi wake kwa baadhi ya hoja.

### 2.1.15 Swali la 15: Uchambuzi wa Machapisho/Maandiko Muhimu ya Kufundishia na Kujifunzia Somo la Uraia

Swali lilimtaka mtahiniwa kufafanua kwa kutumia maarifa aliyopata katika mafunzo yake ya Ualimu, madhumuni sita ya matumizi ya kiongozi cha mwalimu katika kufundisha somo la Uraia.  Kwa ujumla, swali hili lilikuwa

na ufaulu mzuri kwa kuwa asilimia 99.6 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 6 hadi 14.5 kama inavyoonekana katika Chati Na. 15.




**Chati Na. 15:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 15*

Chati Na. 15 inaonesha kuwa, asilimia 0.4 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata kuanzia alama 0 hadi 5.5; asilimia 12.2 walipata kuanzia alama 6 hadi 10 na asilimia 87.4 walipata kuanzia alama 10.5 hadi 14.5.

Uchambuzi unaonesha kuwa, watahiniwa wengi (87.4%) walipata alama za juu katika swali hili kwa sababu walifafanua vema madhumuni ya matumizi ya kiongozi cha mwalimu katika kufundisha somo la Uraia. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ndogo ya Uchambuzi wa Kiongozi cha Mwalimu na walielewa matakwa ya swali. Tofauti kati ya alama zao ilitokana na usahihi wa maelezo ya kila mmoja. Baadhi ya majibu sahihi ya watahiniwa katika swali hili yalikuwa kama ifuatavyo: *kiongozi cha mwalimu huonesha mada ndogo zilizopo kwenye muhtasari, kiongozi cha mwalimu humpa mwalimu maelezo ya kutumia kitabu cha kiada darasani, huonesha majibu ya kazi za kufanywa na wanafunzi na mazoezi yaliyomo kwenye kitabu cha kiada, huonesha muda wa ufundishaji na ujifunzaji, huonesha zana* na *humsaidia mwalimu kujua mawanda na mipaka ya somo husika anapofundisha*. Kielelezo Na. 15.1 ni mfano wa jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri.


15. kiongozi cha mwalimu ni kitabu cha mwalimu ambacho humpa miongozo mbalimbali ya namna ya kufundisha somo la uraia. kiongozi cha mwalimu huwa na madhumuni mbalimbali ambayo humsaidia mwalimu katika mchakato mzima wa ufundishaji. Yafuatayo ni madhumuni ya matumizi ya kiongozi cha mwalimu katika kufundishia somo la uraia.

Humpa mwalimu majibu ya mazoezi ambayo yanapatikana katika kitabu cha kiada. Moja ya madhumuni ya matumizi ya kiongozi cha mwalimu katika kufundisha ni humsaidia mwalimu kwa kumpa majibu ya kile ambacho amefundisha darasani, yaani majibu ya mazoezi ambayo mwalimu hutoa kutoka katika kitabu cha kiada. Mfano majibu ya zoezi la 3.

Humpa mwalimu mbinu mbalimbali ambazo anaweza kutumia katika ufundishaji. Pia dhumuni lingine la matumizi ya kiongozi cha mwalimu katika kufundishia somo la uraia ni pamoja na kumpa mwalimu miongozo ya mbinu mbalimbali ambazo anaweza kutumia kufundishia somo la uraia au mada fulani katika somo hilo. Mfano mbinu ya majadiliano.

Humsaidia mwalimu kumuongoza kupata zana ya kufundishia somo au mada husika katika somo. Pia dhumuni lingine la matumizi ya kiongozi cha mwalimu katika kufundisha somo la uraia ni humsaidia mwalimu kupata ufahamu wa zana ambayo anaweza kutumia kufundishia katika kufanikisha mchakato mzima wa kufundishia. Mfano ramani.

Humuelekeza mwalimu namna ya kuanza kufundisha mada hiyo ya somo la uraia. Dhumuni lingine ni humsaidia mwalimu kwa kumuelekeza namna ambayo anaweza kuanza kufundisha mada hiyo katika somo la



15. uraia. Mfano kueleza dhana ya mahakama.
Humsaidia mwalimu kuweza kubaini zana za upim
aji ambazo anaweza kutumia. Dhumuni lingine la matumizi
ya kiongozi cha mwalimu katika kufundishia somo la urai
a ni pamoja na kumsaidia mwalimu kuweza kubaini zana
za upimaji ambazo anaweza kutumia katika somo hilo la
uraia. Mfano mazoezi.
Humuonesha mwalimu mpangilio wa mada kuu
na mada ndogo ndogo. Pia dhumuni lingine la matumizi
ya kiongozi cha mwalimu ni kumsaidia kupata mpangili
o wa mada kuu na idadi ya mada ndogo zilizomo
kwenye mada kuu. Mfano mada kuu moja ina mada ndog
o tatu.
Hivyo basi, kiongozi cha mwalimu humpa au hu
msaidia mwalimu pale anapokitumia kuweza kufikia m
alengo ya ufundishaji wake katika somo la uraia.

Kielelezo Na. 15.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 15

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, asilimia 12.2 ya watahiniwa waliopata alama za wastani katika swali hili, baadhi yao walishindwa kutoa maelezo yenye kujitosheleza katika kutetea baadhi ya hoja zao na wengine walishindwa kutoa maelezo sahihi ya utangulizi na hitimisho au walitoa majibu pungufu. Mtahiniwa mmoja kwa mfano mbali na kutoa majibu pungufu hakuweza kutoa utangulizi sahihi uliosababisha kukosa alama za kipengele hicho kwa kuandika; *kiongozi cha mwalimu ni kitabu kinachotumika na mwalimu na mwanafunzi ili kufikia malengo mbalimbali ya kielimu nchini*.

Kwa upande mwingine, takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa wachache (0.4%) waliopata kuanzia alama 0 hadi 5.5, baadhi yao walikuwa na maarifa hafifu kuhusu matumizi ya kiongozi cha mwalimu katika kufundisha somo la Uraia na hivyo walishindwa kutoa hoja zilizohitajika. Mtahiniwa mmoja katika kundi hili alipata alama 0 kwa sababu hakuwa na maarifa kuhusu

dhana iliyoulizwa, hivyo kutoa majibu kinyume na swali. Kielelezo Na. 15.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa ambaye ameshindwa kufafanua madhumuni sita ya matumizi ya kiongozi cha mwalimu katika kufundisha somo la Uraia.

15. kiongozi cha mwalimu: ni kitabu kinachotumika na mwa
limu pamoja na mwanafunzi ili kuweza kufikia malengo
ya umahiri husika katika utekelezaji wa maswala
mbali ya kielimu. katika kiongozi cha mwalimu kitabu
hiki kimekuwa na faida kubwa kwani mwalimu anapata
majibu stahiki ya maswali yote. Zifuatazo ni madhumuni
ya matumizi ya kiongozi cha mwalimu.
kuboresha ufundishaji na ujifunzaji: kwa namna mo
ja au nyingine kiongozi cha mwalimu mara nyingi huboresha
ufundishaji wako ili kuweza kukurekebisha na kukusahi
hisha katika maswala mbalimbali ya kielimu hapa
nchini.
Husaidia kufanya Tathmini ya somo husika: mfano
labda ulte somo la uraia kitendo cha kuchunguza ya kuwa
je watoto hao wanauweza katika kufikiri na si kukgelezeana
kazi hivi kitabu hiki cha mwongozo wa mwalimu
husaidia sana katika maswala hayo.
Huamsha ari ya mtoto kujifunza Zaidi: kwa
kawaida kwa matumizi stahiki ya kitabu kile kime
kuwa kikileta motisha chanya zaidi kwao katika pande
hizo mbili kwani ata mwanafunzi pia huweza kukitu
mia katika maswala mbalimbali ya kielimu hapa nchini.
Husaidia katika uandaaji wa Andalio / Azimio la
somo la uraia kwa kawaida katika kiongozi cha mwali
mu ni muhimu sana pia ni nyaraka / vifaa vya
mbavla ... katika Elimu hivyo ivyote husaidia katika


Kielelezo Na. 15.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 15

Kielelezo Na. 15.2 ni sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyeelezea umuhimu wa kutumia mbinu za kufundishia, muhtasari wa somo na zana za kufundishia na kujifunzia katika zoezi zima la ufundishaji na ujifunzaji na

kisha kuziunganisha na kiini cha swali badala ya kufafanua madhumuni ya matumizi ya kiongozi cha mwalimu katika kufundisha somo la Uraia.

### 2.1.16 Swali la 16: Zana za Kufundishia na Kujifunzia

Katika swali hili, mtahiniwa alitakiwa kueleza kwa kutumia hoja tano namna zana za kufundishia na kujifunzia somo la Uraia zinavyoweza kutunzwa. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa asilimia 93.6 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 6 hadi 15 kama inavyoonekana katika Chati Na. 16.




**Chati Na. 16**: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 16*

Chati Na. 16 inaonesha kuwa, asilimia 6.4 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata kuanzia alama 0 hadi 5.5; asilimia 50.4 walipata kuanzia alama 6 hadi 10 na asilimia 43.2 walipata kuanzia alama 10.5 hadi 15.

Takwimu zinaonesha kuwa, nusu ya watahiniwa (50.4%) waliofanya swali hili walipata ufaulu wa wastani. Baadhi ya watahiniwa hao walishindwa kufafanua majibu kwa usahihi na walitoa majibu pungufu. Wengine walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Mtahiniwa mmoja kwa mfano alichanganya majibu yasiyo sahihi kwa kuandika hoja kama; *zihifadhiwe penye usalama*, *zihifadhiwe mashuleni pia*; bila ufafanuzi wa kina. Watahiniwa wengine mbali na dosari mbalimbali walishindwa kutoa maelezo sahihi katika sehemu ya utangulizi na hitimisho na hivyo kupata alama za wastani. Mtahiniwa mmoja kwa mfano aliandika utangulizi usio sahihi kwa kuandika; *zana ni maarifa anayopatiwa mtu au mwanafunzi*

*inaweza kuwa mada ndogo au kubwa*. Mtahiniwa alichanganya maana ya “dhana” na “zana”.


Aidha, asilimia 43.2 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata ufaulu mzuri kwa kuwa walieleza kwa usahihi namna ambavyo zana za kufundishia na kujifunzia zinavyoweza kutunzwa. Tofauti katika alama zao ilitokana na ufasaha katika maelezo ya kila mmoja. Watahiniwa waliopata alama za juu walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ndogo ya Matumizi na Utunzaji wa Zana za Kufundishia na Kujifunzia na walielewa matakwa ya swali. Baadhi ya majibu sahihi ya watahiniwa kwenye swali hili ni; *kuziweka katika makabati maalumu, kuziweka katika masanduku maalumu ya chuma/bati, kuhifadhi katika chumba maalumu cha zana, kuzipaka rangi, kuhifadhi katika mifuko ya plastiki* na *kuning’iniza ukutani au kwenye dari*. Kielelezo Na. 16.1 kinaonesha mfano wa sehemu ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri.

16 au nampa ambavyo unaweza kuhifadhi
au kutunza zana hizo ni:
Kwa kupaka rangi, tunaweza
kuhifadhi zana mbalimbali kwa kupaka
rangi kwani kuna baadhi ya zana
hazifadhiwi bali huzipaka rangi ili
ziweze au zisipate kutu. Mfano: zana
ambazo hutengenezwa kwa chuma au bati.
Kuhifadhi kwenye makabati
kuna zana nyingine ambazo huifadhiwa
kwenye makabati ili zisiweze kupata
vumbi, Mfano televisheni na Radio.
Huhifadhiwa kwenye maboksi
Baadhi ya zana huifadhiwa kwenye
maboksi ili zisichanike au kutupwa
hii husaidia katika kuhifadhi, Mfano
wa zana hizo ni majarida
mbalimbali na kadi mbalimbali.
huweza kuhifadhiwa kwenye
vyumba maalumu, pia zana hizo
huweza kuhifadhiwa kwenye vyumba
maaluma mfano maabara ambapo
huifadhi vitaa mbalimbali.
Kwa kuwekewa fremu, pia
zana huweza kuwekewa fremu ili zisipa
te kutu au unyevu unyevu, Mfano picha
mbalimbali
Hivyo basi, hizo ni njia ambazo
hutumika katika kuhifadhi zana za
kufundishia na kujifunzia ambazo
huweza kurahisisha suala zima la
ufundishaji na ujifunzaji.

Kielelezo Na. 16.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 16

Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache (6.4%) waliopata kuanzia alama 0 hadi 5.5, baadhi yao walikuwa na maarifa hafifu kuhusu dhana ya Utunzaji wa zana za kufundishia na kujifunzia na hivyo walishindwa kutoa idadi ya majibu iliyohitajika na maelezo ya kina katika kutetea majibu hayo. Mtahiniwa mmoja aliyepata alama 0 hakuelewa matakwa ya swali hivyo

aliandika majibu kinyume na matakwa ya dhana iliyoulizwa kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 16.2.


kujifunzia na kufundishia somo la uraia zinavyoweza kutunzwa.

Kuzitengeneza zinapoharibika, kwa njia hii zana za kufundishia na kujifunzia somo la uraia zinaweza kutunzwa na kudumu kwa muda mrefu.

16. Kuzisafisha baada ya matumizi, ili zana za kufundishia na kujifunzia somo la uraia ziweze kwa umara lazima zisafishwe baada ya kutumika.

Kuzirudisha mahala pake baada ya matumizi, zana zinapo malizika kutumiwa lazima zikahifadhiwe sehemu salama ambapo zitaweza kukaa bila ya kubugudhiwa na kitu chochote.

Kuzihamisha au kuzibeba, kwa umakini kama ni zana za kuvunjika kwa haraka hivyo zikibebwa kwa umakini zitasaidia katika kuzitunza kwa umakini.

Kuziandalia mazingira salama kwa ajili ya kuzitunza, na kuzitumia, mfano unaweza zibandika au ukaweka juu ya meza iliyokaa vizuri ili zisiweze kudondoka na kuharibika.

Kwa mfano zana zinapopata mipasuko na majeraha mbalimbali unaweza ukazirudia kwa kuzipaka rangi au kupigilia pamoja na kuongeza udongo kama ni zana ya udongo.

Kielelezo Na. 16.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 16

Katika Kielelezo Na. 16.2 mtahiniwa alieleza mambo ya kuzingatia katika kutumia zana za kufundishia na kujifunzia kwa majibu kama; *kuzitengeneza zinapoharibika*, *kuzisafisha baada ya matumizi* na *kuzirudisha mahala pake* badala ya kueleza namna zana za kufundishia na kujifunzia somo la Uraia zinavyoweza kutunzwa.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA

Mtihani wa somo la Uraia ulitahini mada tisa (9) ambapo mada nane (8) kati ya hizo zilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu. Mada hizo ni: *Uchambuzi wa Maandiko/Machapisho Muhimu ya Kufundishia na Kujifunzia Somo la Uraia* (99%), *Upimaji na Tathmini* (97.8%), *Uchumi wa Tanzania* (95.9%), *Maandalizi ya Kufundishia Somo la Uraia* (94.8%), *Zana za Kufundishia Somo la Uraia* (92.8%), *Utamaduni Wetu* (90.5%), *Uhusiano wa Kimataifa* (88.7%) na *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la Uraia* (76.6%) kama kiambatisho kinavyoonesha. Ufaulu huu umesababishwa na watahiniwa wengi kuwa na ujuzi na weledi wa kutosha kuhusu mada hizo.

Hata hivyo, mada ya *Dola* ambayo ilitahiniwa katika swali la 1, 2, 5 na 11 ilikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu wa asilimia 66.6 kwa sababu watahiniwa wengi hawakuwa na umahiri wa kutosha katika kuandika hoja zenye mtiririko mzuri kimantiki.

## 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika somo hili ni mzuri kwa kuwa asilimia 99.95 ya watahiniwa walifaulu. Sababu mbalimbali zimeainishwa kuelezea ufaulu huo kama; kuwa na maarifa ya kutosha katika dhana mbalimbali zilizoulizwa, umahiri wa kutosha katika kuandika hoja zenye mtiririko mzuri kimantiki na kuwa na umakini katika kusoma na kuelewa matakwa ya swali. Hata hivyo, ili kuimarisha ufaulu zaidi juhudi zinahitajika katika matumizi ya mbinu sahihi za kufundishia na kujifunzia kama; majadiliano ya vikundi na uwasilishaji, kusoma kwa vikundi vitabu na matini mbalimbali kwa kutumia maktaba na mtandao wa intaneti, kuwahoji watu mbalimbali, midahalo na kwa kualika mgeni hususan kwenye mada ya Dola iliyokuwa na ufaulu wa wastani.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuinua zaidi ufaulu wa wanachuo katika somo hili inapendekezwa kuwa:

(a) Mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji utumie zaidi mbinu shirikishi hususan mbinu ya majadiliano. Hii itawasaidia wanachuo kujenga uelewa na kutunza kumbukumbu ya maarifa wanayoyapata. Pia itawajengea uwezo wa kuwasilisha mawazo yao katika miktadha mbalimbali hivyo kuwajengea uwezo wa kujibu maswali vizuri na kufaulu katika mitihani yao.

(b) Wanachuo wanashauriwa kusoma vitabu na matini mbalimbali ili kuweza kupata maarifa yaliyokusudiwa hususan katika dhana ya Dola iliyokuwa na ufaulu wa wastani.

(c) Wakufunzi watoe majaribio, mazoezi ya kutosha na mrejesho sahihi hususan kwenye mada ambayo ilikuwa na ufaulu wa wastani ya Dola ili kuboresha kiwango cha ufaulu.

(d) Wakufunzi wawaelekeze wanachuo kuhusu namna ya kujibu maswali vizuri kwa kuzingatia aina ya swali na kuwasisitiza kuwa na umakini katika kusoma na kubaini matakwa ya swali kabla ya kuanza kujibu.

*Kiambatisho*

## MUHTASARI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA SOMO LA URAIA

| Na. | Mada | Na. ya Swali | Ufaulu Katika Kila Swali (%) | Wastani wa Ufaulu Katika Kila Mada (%) | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Uchambuzi wa Maandiko/Machapisho Muhimu ya Kufundishia na Kujifunzia Somo la Uraia | 6 | 98.3 | 99 | Vizuri |
| | | 15 | 99.6 | | |
| 2. | Upimaji na Tathmini | 9 | 98.1 | 97.8 | Vizuri |
| | | 10 | 97.4 | | |
| 3. | Uchumi wa Tanzania | 4 | 95.9 | 95.9 | Vizuri |
| 4. | Maandalizi ya Kufundisha Somo la Uraia | 8 | 94.8 | 94.8 | Vizuri |
| 5. | Zana za Kufundishia na Kujifunzia | 7 | 92 | 92.8 | Vizuri |
| | | 16 | 93.6 | | |
| 6. | Utamaduni Wetu | 3 | 81.4 | 90.5 | Vizuri |
| | | 12 | 99.5 | | |
| 7. | Uhusiano wa Kimataifa | 13 | 88.7 | 88.7 | Vizuri |
| 8. | Misingi ya Ufundishaji wa Somo la Uraia | 14 | 76.6 | 76.6 | Vizuri |
| 9. | Dola | 1 | 98.9 | 66.6 | Wastani |
| | | 2 | 70.2 | | |
| | | 5 | 5.4 | | |
| | | 11 | 92 | | |